# Ilani kuhusu Desturi za Faragha

**Tumejitolea Kulinda Faragha Yako**
Tunaipa kipaumbele faragha ya taarifa zako za kiafya katika Corewell Health. Ilani hii inawapa wagonjwa na familia za Corewell Health maelezo kuhusu haki zao za faragha na juhudi zinazoendelea za Corewell Health za kulinda haki hizo. Una haki ya kufanya uamuzi kuhusu jinsi taarifa zako za kiafya zinavyokusanywa na kutumiwa.

**Maswali na Masuala**
Corewell Health, Chief Privacy Officer MC168, 100 Michigan Street NE, Grand Rapids, MI 49503
• Simu: **616.486.4113**
• Barua pepe: **privacy@corewellhealth.org**

**Ilani ya Jumla ya Desturi za Faragha**
Ilani hii inafafanua jinsi taarifa za kimatibabu zinazokuhusu zinavyoweza kutumiwa na kufumbuliwa na jinsi unavyoweza kufikia taarifa hizi. **Tafadhai kagua ilani hii kwa umakini**. Ilani hii ilianza kutumika tarehe 17 Agosti 2023.

Iwapo una maswali kuhusu ilani hii, wasiliana na Afisa Mkuu wa Faragha (Chief Privacy Officer) wa Corewell Health kupitia **privacy@corewellhealth.org** au ukitumia maelezo ya mawasiliano yaliyoorodheshwa hapo juu.

**Ni Nani Atafuata Ilani Hii**
Ilani hii inatumiwa na "Corewell Health" au "vituo vya Corewell Health" vikiwemo hospitali, vituo vya huduma kwa wakongwe, vituo vya huduma za dharura, wahudumu wetu wa matibabu, mashirika ya kutoa huduma za kiafya nyumbani, hospitali za magonjwa ya kudumu, kliniki, afisi na vituo vinavyosimamiwa na Corewell Health. Vituo na ofisi zote za Corewell Health zitafuata ilani hii, ziwe zimeorodheshwa au hazijaorodheshwa. Mabadiliko katika Ilani hii ya Desturi za Faragha inapatikana katika ofisi au kituo ambako unapokea huduma, kwa kupiga simu kwa **616.486.4113**, au kwa kutuma barua pepe kwa **privacy@corewellhealth.org**.
Ilani hii pia inatumiwa na mashirika yaliyo katika Mpango wa Matibabu Yaliyoratibiwa (OHCA, Organized Health Care Arrangement) wa Corewell Health. Mashirika haya yatashiriki taarifa zako za kiafya zinazolindwa (PHI) kati yao kwa madhumuni ya matibabu, malipo na huduma za kiafya.

Corewell Health inahifadhi haki ya kubadilisha kushiriki kwa mtu au shirika lolote katika mpango wake wa OHCA. Iwapo una maswali kuhusu kushiriki kwa mtoa huduma za kiafya katika mpango wa OHCA, piga simu kwa nambari **616.486.4113** au tuma barua pepe kwa **privacy@corewellhealth.org**.

**Ahadi Yetu Kuhusu Taarifa Zako za kiafya**
Tunaelewa kuwa taarifa zako za kiafya ni za binafsi, na tumejitolea kuzilinda. Taarifa za kiafya tunazotumia, kubuni, kuhifadhi na kufumbua kukuhusu zinaweza kuhusiana na huduma za kiafya ya kimwili na ya kiakili tunayokupa. Tunaandaa rekodi ya matibabu na huduma unazopokea katika Corewell Health. Rekodi hii inaturuhusu kukupa huduma bora na kutii masharti fulani ya kisheria. Ilani hii inatumiwa kwenye rekodi zote zinazohusiana na huduma yako, zinazohifadhiwa katika Corewell Health, ziwe za kielektroniki au za karatasi. Iwapo daktari anayekuhudumia hatoki Corewell Health, anaweza kuwa na sera au ilani tofauti kuhusu matumizi na ufumbuzi wa taarifa zako za matibabu. Ilani hii inakufahamisha kuhusu njia ambazo taarifa zako za faragha hutumiwa na kufumbuliwa. Inafafanua pia haki na wajibu wako kuhusu utumiaji na ufumbuzi wa taarifa za kiafya.

Kwa mujibu wa sheria, tunatakiwa:
• Kudumisha faragha na usalama wa PHI zako.
• Kufuata desturi za faragha zilizofafanuliwa katika ilani hii na kukupa nakala yake.
• Kuwaarifu walioathiriwa kutokana na kufichuliwa kwa taarifa za kiafya ambazo hazijalindwa.

**Jinsi Tunavyoweza Kutumia na Kufumbua Taarifa Zako za kiafya**
Katika hali nyingi, tunaweza kutumia na kufumbua taarifa zako za kiafya bila ruhusa yako iliyoandikwa. Hata hivyo, utumiaji na ufumbuzi ambao haujafafanuliwa hapa chini utafanywa tu kupitia ruhusa yako iliyoandikwa. Katika hali fulani, idhini yako iliyoandikwa inahitajika ili kutumia au kufumbua taarifa zako za kiafya. Kwa mfano, hatutawahi kuuza au kutumia taarifa zako kwa madhumuni ya utangazaji bila ruhusa yako. Vitengo vifuatavyo vinafafanua njia tofauti ambazo tunatumia na kufumbua taarifa za kiafya.

**Kwa Ajili ya Matibabu:** Tunaweza kutumia taarifa zako za kiafya na kuzifumbua kwa wataalamu wengine wanaokutibu.
Kwa mfano, daktari anayekutibu jeraha akimwuliza mtoa huduma mwingine wa afya kuhusu hali ya afya yako kwa jumla.
Tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa madhumuni ya kuendeleza huduma za matibabu. Idara tofauti za Corewell Health zinaweza kufumbua taarifa zako za kiafya ili kuratibu mambo tofauti unayohitaji, kama vile maagizo ya dawa, kazi za maabara, eksrei, au matibabu, au kupanga rufaa.
Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kukuhusu kwa wahudumu wasio wa Corewell Health wanaohusika katika huduma yako ya afya baada ya matibabu katika Corewell Health, kama vile wanafamilia au watoa huduma za kiafya nyumbani. Tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa mtoa huduma mwingine wa afya utakayeelekezwa kwake kwa ajili ya huduma za kiafya.
Watoa huduma za kiafya wanaokutibu nje ya Corewell Health wanahitaji kupata taarifa kamili iwezekanavyo ili kufanya maamuzi kuhusu huduma yako. Watoa huduma hawa wanaweza kupata rekodi zako za kielektroniki na za karatasi kutoka Corewell Health kwa

madhumuni haya. Pia, wakati watoa huduma hawa wamekuelekeza kwenye Corewell Health kwa ajili ya matibabu, wanaweza pia kufikia rekodi na taarifa zako za kiafya ili kufuatilia hatua za matibabu yako. Corewell Health ina taratibu na teknolojia za kulinda faragha na usalama wa rekodi zako katika hali hizi.

**Kwa Ajili ya Malipo:** Tunaweza kutumia na kufumbua taarifa zako za kiafya na taarifa zisizo za kiafya ili kutoza na kupokea malipo kutoka katika mipango ya afya au taasisi nyingine za matibabu na huduma unazopokea katika Corewell Health. Kwa mfano, tunaweza kutoa taarifa kuhusu wewe kwenye mpango wako wa bima ya afya ili ilipie matibabu au huduma unazopokea. Tunaweza kuwasiliana na mpango wako wa afya kuhusu matibabu utakayopokea ili kupata idhini ya mapema au kubaini iwapo mpango wako utashughulikia matibabu. Baadhi ya watoa huduma za kiafya katika Corewell Health hutoza kivyao na tunaweza kuwapa taarifa zinazohusu malipo ili kuratibu mchakato wa kutoza na malipo. Tunaweza pia kuwasiliana nawe kupitia barua au simu ili kujadili akaunti yako au kuthibitisha au kupata maelezo zaidi kuhusu bima yako ya afya. Iwapo umelipia bidhaa au huduma ya afya kikamilifu, na utufahamishe kuwa hungependa mpango wako wa afya upokee taarifa kuhusu bidhaa au huduma hiyo, hatutafumbua taarifa hizo kwa mpango wako wa afya, isipokuwa zitakikane kwa mujibu wa sheria.

**Kwa Ajili ya Huduma za kiafya:** Tunaweza kutumia na kufumbua taarifa zako za kiafya ili kutekeleza kazi yetu—kama vile za kiuhasibu, kushughulikia madai, au kutathmini waajiriwa wetu. Utumiaji na ufumbuzi huu unahitajika ili kutekeleza shughuli za kikazi za Corewell Health na kuhakikisha kuwa wagonjwa wetu wote wanapokea huduma bora za kiafya. Kwa mfano, tunaweza kufumbua taarifa zako kwa Priority Health, mpango wa afya unaomilikiwa na Corewell Health, kama sehemu ya Mpango wetu wa Huduma ya Afya Iliyoratibiwa (OHCA). Kushiriki taarifa na Priority Health hutusaidia kutimiza madhumuni ya mfumo wetu wa jumla wa afya, kama vile kuimarisha ubora, kudhibiti afya ya watu, na kuboresha afya na siha ya jumuiya zinazohudumiwa na Corewell Health na Priority Health. Tunaweza pia kutumia taarifa fulani za kimatibabu na zisizo za kimatibabu kuwasiliana nawe na kuomba maoni yako kuhusu ubora wa huduma ulizopokea katika Corewell Health na jinsi tunavyoweza kuboresha huduma zetu. Tunaweza pia kujumuisha taarifa za kiafya kuhusu wagonjwa wengi ili kuamua huduma za ziada ambazo Corewell Health inapaswa kutoa, huduma ambazo hazihitajiki na kubaini iwapo matibabu mapya yanafaa. Tunaweza kufumbua taarifa kwa madaktari, wauguzi, mafundi, wanafunzi wa taaluma ya matibabu na wafanyakazi wengine wa hospitali kwa madhumuni ya kielimu. Tunaweza kujumuisha taarifa za kiafya tulizo nazo pamoja na taarifa za kiafya kutoka kwa mashirika mengine ili kulinganisha utendaji wetu na kubaini jinsi tunavyoweza kuboresha matibabu na huduma zetu.

**Utumiaji na Ufumbuzi Kulingana na Hali:** Tunaweza kutumia au kufumbua taarifa zako za kiafya zinapohusishwa na utumiaji au ufumbuzi mwingine unaoruhusiwa au kutakiwa kisheria. Kwa mfano, mazungumzo kati ya madaktari, wauguzi au wataalamu wengine wa Corewell Health kuhusu hali yako ya kiafya yanaweza kufichuliwa wakati mwingine. Tunakuhakikishia kuwa tumeweka mikakati ya kuzuia hali kama hizo kadri tuwezavyo.

**Vikumbusho vya Miadi:** Tunaweza kutumia na kufumbua taarifa za kiafya illi kukukumbusha kuhusu miadi ijayo katika kituo cha Corewell Health au umuhimu wa kupata maagizo mapya ya dawa.

**Shughuli za Kuchangisha Pesa:** Katika hali ya kuchangisha pesa, tunaweza kutumia taarifa fulani zisizo za matibabu, zikiwemo jina lako, anwani, nambari ya simu, tarehe na mahali pa huduma, umri, na jinsia ili kuwasiliana nawe uchangishe pesa kwa ajili ya washirika wa Corewell Health kupitia shirika linalomilikiwa au kusimamiwa na Corewell Health. Pesa zinazochangishwa zitatumiwa kupanua na kuboresha huduma na mipango yetu kwa jumuiya. Una haki ya "kujiondoa" katika mpango wa utumiaji na ufumbuzi wa taarifa zako kwa madhumuni ya kuchangisha pesa.

**Saraka ya Hospitali:** Tunaweza kujumuisha taarifa chache kuhusu wewe katika saraka ya hospitali ukiwa mgonjwa katika hospitali ya Corewell Health. Taarifa hizi zinaweza kujumuisha jina lako, eneo uliko hospitalini, hali yako ya jumla (mfano, nafuu, kawaida, nk.), na dini yako. Taarifa hizi, isipokuwa dini yako, zinaweza pia kufumbuliwa kwa watu wanaokuulizia kwa kutaja jina lako. Aidha, hospitali inaweza kuhifadhi saraka tofauti inayoorodhesha dini yako na kufumbua saraka hiyo kwa viongozi wako wa kidini. Tunafanya hivyo ili familia, marafiki na viongozi wako wa kidini waweze kukutembelea hospitalini na kujua hali yako ya jumla. Una haki ya kutuambia kuzuia (kudhibiti au kutojumuisha) taarifa zako katika saraka za hospitali. Ili tuzuie taarifa hizo, ni lazima utufahamishe wakati wa kujisajili.

**Wanaohusika katika Huduma Yako au Malipo ya Huduma Yako:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu kwa rafiki au mwanafamilia anayehusika katika huduma yako mradi hujakataa, au iwapo tunaamini ufumbuzi huo ni kwa manufaa yako. Tunaweza pia kutoa taarifa kwa mtu yeyote ambaye anahusika katika malipo au anasaidia kulipia huduma yako. Tunaweza kuwafahamisha familia na marafiki zako kuhusu hali yako kwa jumla. Aidha, tunaweza kufumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu kwa taasisi inayosaidia kutoa msaada kutokana na janga, ili familia yako iweze kuarifiwa kuhusu hali na mahali uliko.

**Utafiti:** Katika hali fulani, tunaweza kutumia na kufumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu kwa madhumuni ya utafiti. Kwa mfano, mradi wa utafiti unaweza kujumuisha kutathmini afya na nafuu kwa wagonjwa waliopokea matibabu ya aina moja ikilinganishwa na waliopokea matibabu mengine

katika mazingira sawa. Miradi yote ya utafiti hupitia mchakato maalum ya uidhinishaji. Mchakato huu hutathmini mradi uliopendekezwa wa utafiti na matumizi yake ya taarifa za kiafya. Mchakato huu pia huhakikisha kuwa mahitaji ya utafiti yanalingana na mahitaji ya wagonjwa wetu kuhusu faragha ya taarifa zao za kiafya. Kabla tutumie au kufumbua taarifa za kiafya kwa ajili ya utafiti, mradi huo utakuwa umekaguliwa kupitia mchakato huu wa kuidhinisha utafiti.  Hata hivyo, tunaweza kufumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu kwa watu wanaojiandaa kutekeleza mradi wa utafiti. Kwa mfano, tunaweza kufumbua taarifa kwa watafiti ili kuwasaidia kutafuta wagonjwa wenye mahitaji maalum ya kimatibabu, mradi taarifa wanazokagua hazitoki nje ya Corewell Health. Tunaweza kuomba ruhusa yako mahususi iwapo mtafiti atatumia jina, anwani, au taarifa zako nyingine za binafsi, au atahusika katika huduma inayohusiana na utafiti katika Corewell Health.

**Kwa Mujibu wa Sheria:** Tutafumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu tunapotakiwa kufanya hivyo na serikali, jimbo, au sheria au kanuni za eneo mahususi. Kwa mfano, tunatakiwa kuripoti majeraha au magonjwa fulani kwa madhumuni ya afya ya umma.

**Ili Kuepuka Tisho Kubwa kwa Afya au Usalama:** Tunaweza kutumia na kufumbua taarifa zako za kiafya panapohitajika ili kuzuia tisho kubwa kwa afya au usalama wako, wa umma au wa mtu mwingine. Tutafumbua tu taarifa zako kwa mtu aliye na uwezo wa kuzuia tisho hilo.

**Mawasiliano Kuhusu Bidhaa au Mipango ya Corewell Health:** Tunaweza kutumia na kufumbua taarifa za kiafya ili kukufahamisha kuhusu huduma au bidhaa inayohusiana na afya katika Corewell Health. Isitoshe, tunaweza kutumia au kufumbua taarifa zako za kiafya ili kukufahamisha kuhusu bidhaa au huduma zinazohusiana na matibabu yako, kudhibiti mgonjwa au kuratibu huduma, au kutoa mawasiliano kuhusu njia mbadala za matibabu, tibamaungo, watoa huduma, au mazingira ya huduma. Mara kwa mara, tunaweza kukufahamisha kuhusu bidhaa au huduma za kampuni nyingine lakini tutatumia au kufumbua taarifa zako za kiafya kwa ajili ya mawasiliano kama hayo iwapo tu yatafanyika ana kwa ana.

**Mawasilisho ya Taarifa za kiafya:** Corewell Health hurekodi na kutuma taarifa za kiafya, yakiwemo maagizo ya dawa, kwa njia ya kielektroniki. Taarifa za kiafya hushirikiwa kwa njia ya kielektroniki kwa madhumuni yaliyobainishwa katika ilani hii na hulindwa kupitia mawasilisho ya taarifa za kiafya ya kimaeneo, ya jimbo na ya kitaifa. Corewell Health hushiriki katika mawasilisho ya taarifa za kiafya, ikiwemo MiHIN (Mtandao wa Taarifa za kiafya wa Michigan), na inaweza kushiriki katika mawasilisho mengine ya taarifa baadaye. MiHIN ina sheria kuhusu jinsi taarifa za kiafya zinavyoweza kufikiwa kupitia mawasilisho na hudhibiti utumiaji na ufumbuzi wa taarifa kama hizo. Unaweza kutuma barua pepe kwa **privacy@corewellhealth.org** kwa maelezo zaidi kuhusu MiHIN na haki zako zinazohusishwa na kutuma taarifa zako kupitia hili na mawasilisho mengine ya taarifa za kiafya.

**Epic's Care Everywhere:** Rekodi yako ya matibabu huhifadhiwa kwa njia ya kielektroniki katika Epic, ambayo ni programu ya kompyuta. Ili kuboresha huduma unayopokea, Corewell Health hushiriki rekodi zako za kiafya kwa njia ya kielektroniki na watoa huduma wengine kwa kutumia Epic's Care Everywhere. Tunafanya hivyo ili kuruhusu watoa huduma wengine wa afya wanaotumia Epic na wanaokutibu kuona taarifa zako za matibabu mara moja. Wakati umesajiliwa katika hospitali nyingine inayotumia Epic, daktari anayekutibu katika hospitali hiyo anaweza kuomba rekodi za matibabu kutoka kwa hospitali yetu kwa njia ya kielektroniki. Kwa mfano, katika hali ya dharura, daktari anaweza kuomba rekodi yako ya matibabu kutoka Corewell Health kwa njia ya kielektroniki kisha, iwapo atapewa "ruhusa," ataangalia matokeo yako ya maabara. Kushiriki taarifa zako za kiafya kwa njia hii kunaweza kumwezesha daktari kufanya maamuzi bora ya matibabu. Tumeweka mikakati ya usalama ili kuhakikisha kuwa kwa sasa unapokea huduma katika hospitali au mtoa huduma za kiafya anayeomba taarifa hizo. Lazima watoa huduma za kiafya wawe na taarifa za kutosha kukuhusu ili kuthibitisha kuwa wanatoa huduma kwako NA ni lazima ujisajili kama mgonjwa katika rekodi yao ya matibabu ya kielektroniki. Taarifa zako za kiafya zinaweza kujumuisha utambuzi nyeti kama vile HIV/Ukimwi, magonjwa ya zinaa, maelezo ya kijenetiki, afya ya kiakili, matumizi ya dawa za kulevya, vipimo vya kijenetiki, nk. Maelezo ya tiba ya akili hayajumuishwi katika rekodi yako ya matibabu au mawasilisho yetu ya taarifa za kiafya. Iwapo ungependa "kujiondoa" kwenye Epic's Care Everywhere, tafadhali wasiliana na Ofisi yetu ya Faragha kupitia nambari ya simu au anwani ya barua pepe iliyoorodheshwa katika safu wima ya kwanza ya ilani hii.

## Jinsi Tunavyoweza Kutumia au Kufumbua Taarifa Zako za Kiafya – Hali Maalum

Katika hali nyingi, tunaweza kutumia na kufumbua taarifa zako za kiafya bila ruhusa yako iliyoandikwa. Maelezo yafuatayo yanabainisha jinsi tunavyoweza kutumia au kufumbua taarifa zako za kiafya katika hali maalum.

**Kutoa Mchango wa Viungo na Tishu:** Iwapo wewe ni mmoja wa wanaotoa mchango wa kiungo fulani cha mwili, tunaweza kufumbua taarifa za kiafya, panapohitajika, kwa mashirika yanayoshughulikia ununuzi wa viungo, au upandikizaji wa jicho, kiungo na tishu, au kwenye hifadhi ya mchango wa viungo.

**Jeshi na Wanajeshi Waliostaafu:** Iwapo wewe ni mwanajeshi, tunaweza kufumbua taarifa za matibabu zinazokuhusu kwa mujibu wa mamlaka ya amri za wanajeshi. Tunaweza pia kufumbua taarifa za kiafya kuhusu wanajeshi wa kigeni kwa mamlaka inayofaa ya wanajeshi wa kigeni. Iwapo mwanafamilia ni mwanajeshi, katika hali fulani, tunaweza kufumbua taarifa kukuhusu kwa jeshi au taasisi iliyoidhinishwa ya

huduma za kijamii kama vile Msalaba Mwekundu (Red Cross) ili kutoa ushauri kwa mwanafamilia yako kuhusu hali yako.

**Fidia kwa Wafanyakazi:** Tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa mpango wa fidia kwa wafanyakazi au mipango kama hiyo. Mipango hii hutoa fidia kwa magonjwa na majeraha yanayohusiana na kazi.

**Hatari kwa Afya ya Umma:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kuhusu wewe kwa ajili ya huduma za kiafya ya umma, zikiwemo:
- Kuzuia au kudhibiti magonjwa, majeraha au ulemavu.
- Kuripoti visa vya kuzaliwa na vifo na kushiriki katika sajili za magonjwa.
- Kuripoti kisa cha kutelekezwa au kunyanyaswa kwa watoto.
- Kuripoti athari za dawa au matatizo ya bidhaa.
- Kuwaarifu watu kuhusu kurejesha bidhaa ambazo huenda wanatumia.
- Kumwarifu mtu ambaye huenda ameathiriwa na ugonjwa au yuko katika hatari ya kupata au kusambaza ugonjwa au hali fulani.
- Kuarifu mamlaka yanayofaa ya serikali iwapo tunaamini kuwa mgonjwa ni mwathiriwa wa tukio la unyanyasaji, kutelekezwa, au vurugu ya kifamilia. Tutafanya ufumbuzi huu tu iwapo utakubali, au wakati ukitakikana au kuidhinishwa kisheria.

**Shughuli za Uangalizi wa Afya:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kwa taasisi ya uangalizi wa afya kwa ajili ya shughuli zinazoruhusiwa kisheria. Shughuli hizi za uangalizi ni pamoja na, kwa mfano, ukaguzi wa mahesabu, uchunguzi, upelelezi na utoaji wa leseni. Shughuli hizi zinahitajika ili serikali ifuatilie mfumo wa huduma ya afya, mipango ya serikali na utiifu wa haki za kiraia.

**Kesi na Mizozo:** Iwapo unahusika katika kesi au mzozo, tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kukuhusu tukiagizwa na korti au amri ya mahakama. Tunaweza pia kufumbua taarifa za matibabu zinazokuhusu kutokana na agizo la mahakama, ombi la ugunduzi au mchakato mwingine wa kisheria wa mtu mwingine anayehusika katika mzozo. Tutafanya hivyo tu iwapo umekubali. Hata hivyo, ruhusa yako haitahitajika iwapo ombi la ufumbuzi limetiwa saini na hakimu au limeagizwa na mahakama.

**Kutekeleza Sheria:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kwa afisa wa kutekeleza sheria katika hali zifuatazo:
Kutii agizo la korti, amri ya mahakama, dhamana, maagizo ya kufika mahakamani au michakato kama hiyo,
- Ili kutambua au kujua aliko mshukiwa, mtoro, shahidi muhimu au mtu aliyepotea,
- Iwapo taarifa zinahusu mwathiriwa wa uhalifu, na iwapo, katika hali fulani, hatuwezi kupata idhini ya mtu huyo ya ufumbuzi,
- Kuhusu kisa cha kifo ambacho tunaamini kinaweza kutokana na matendo ya uhalifu,
- Kuhusu matendo ya uhalifu katika kituo cha Corewell Health, au
- Katika hali za dharura ili kuripoti uhalifu, waathiriwa au eneo la uhalifu, au utambulisho (maelezo au eneo) wa mtu aliyetekeleza uhalifu.

**Wapelelezi wa Vifo, Wakaguzi wa Matibabu na Wasimamizi wa Mazishi:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya kwa mpelelezi wa kifo au mkaguzi wa matibabu. Hili linaweza kuhitajika, kwa mfano, ili kumtambua aliyefariki au kubaini chanzo cha kifo. Tunaweza pia kufumbua taarifa za matibabu kuhusu wagonjwa kwa wasimamizi wa mazishi, panapohitajika, ili wafanya kazi zao.

**Shughuli za Ujasusi na Usalama wa Kitaifa:** Tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa maafisa walioidhinishwa wa serikali kwa ajili ya ujasusi, ulinzi wa wajasusi na shughuli nyingine za usalama wa kitaifa zilizoidhinishwa kisheria.

**Huduma za Ulinzi kwa Rais na Wengine:** Tunaweza kufumbua taarifa za kiafya zinazokuhusu kwa maafisa walioidhinishwa wa serikali ili waweze kumlinda rais, watu walioidhinishwa au marais wa kigeni, au kufanya upelelezi maalum.

**Wafungwa:** Iwapo wewe ni mfungwa kwenye gereza au chini ya ulinzi wa polisi, tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa gereza au polisi husika. Ufumbuzi huu unaweza kuhitajika ili taasisi hiyo ikupe huduma za kiafya, kulinda afya na usalama wako au afya na usalama wa wengine, au kwa usalama wa gereza na ulinzi wa taasisi za kurekebisha tabia.

**Washirika Wengine:** Tunaweza kufumbua taarifa zako za kiafya kwa washirika wengine ambao tunaweka nao mkataba wa kutekeleza huduma kwa niaba ya taasisi ya Corewell Health. Hilo likifanyika, tutakuwa na mwafaka ulioandikwa kutoka kwa shirika hilo lingine kuwa taarifa zako zitalindwa.

**Taarifa za Siri Zaidi:** Taarifa fulani za kiafya hupokea ulinzi maalum wa faragha, kama vile madokezo ya tiba ya kiakili, huduma za kiafya ya akili na ulemavu wa kukua, huduma za kutibu na kuzuia matumizi ya dawa za kulevya na pombe, na magonjwa fulani. Tutatumia au kushiriki tu taarifa zako za matibabu zilizo za siri zaidi tukiwa na ruhusa au tukihitajika kisheria, au ukitupa ruhusa yako kwa maandishi.

## Haki Zako Kuhusu Taarifa Zako za kiafya

**Haki ya Kukagua na Kunakili:** Unaweza kuomba kuona au kupata nakala ya kielektroniki au halisi ya rekodi yako ya matibabu na taarifa nyingine za kiafya tulizo nazo zinazokuhusu. Taarifa zinazopatikana kwako ni pamoja na rekodi za malipo na matibabu lakini hazijumuishi maelezo yoyote ya tiba ya kiakili. Uliza Usimamizi wa Taarifa za kiafya (HIM, Health Information Management) jinsi ya kufanya hivyo. Tutakupa nakala au muhtasari wa taarifa zako za kiafya, kwa kawaida ndani ya siku 30 baada ya kutuma ombi. Tunaweza kukutoza ada fulani. Tunaweza kukataa ombi lako la kukagua na kunakili katika hali

fulani chache. Iwapo hatutakuruhusu ufikie taarifa za kiafya, unaweza kuomba uamuzi huo ukaguliwe. Mtaalamu mwingine aliyeidhinishwa wa huduma za kiafya atakayechaguliwa na Corewell Health atakagua ombi lako na uamuzi wa kulikataa. Atakayefanya ukaguzi siye aliyekataa ombi lako la kwanza. Tutatii matokeo ya ukaguzi. Iwapo unashiriki katika shughuli za utafiti, tunaweza kukataa ombi lako la kukagua na kunakili baadhi ya taarifa zako za kiafya zinazohusiana na utafiti huo, mradi ulikubali udhibiti huu wa ufikiaji katika fomu ya idhini uliyotia saini kabla ya kushiriki. Tunaweza pia kukuzuia usipate taarifa jinsi ilivyobainishwa kisheria.

**Haki ya Kurekebisha:** Unaweza kuomba HIM irekebishe taarifa zako za kiafya ambazo unafikiri si sahihi au si kamili. Tuulize jinsi ya kufanya hili. Tunaweza "kukataa" ombi lako, lakini tutakupa sababu ndani ya siku 60 kwa maandishi. Tunaweza kukataa ombi lako la kurekebisha iwapo halijaandikwa au halijumuishi sababu ya ombi hilo. Tunaweza pia kukataa ombi lako ukituomba turekebishe taarifa ambazo:

- Hatukutunga, isipokuwa mtu au taasisi iliyotunga taarifa hizo haipatikani ili kufanya marekebisho.
- Si sehemu ya taarifa za kiafya zinazohifadhiwa na, au kwa ajili ya taasisi ya Corewell Health.
- Si sehemu ya taarifa ambazo unaruhusiwa kukagua na kunakili.
- Ni sahihi na kamilifu.

**Haki ya Orodha ya Matukio ya Ufumbuzi:** Unaweza kuomba orodha (matukio) ya mara ambazo tumeshiriki taarifa zako za kiafya kwa miaka sita kabla ya tarehe unayotuma ombi, tuliyeshiriki naye, na sababu ya kushiriki. Uliza HIM jinsi ya kutuma ombi la hili. Tutajumuisha matukio yote ya ufumbuzi isipokuwa unaohusu matibabu, malipo, na huduma za kiafya, na ufumbuzi mwingine (kama vile wowote uliotuomba tufanye). Tutatoa orodha moja kwa mwaka bila malipo, lakini tutatoza ada kulingana na gharama iwapo utaomba orodha nyingine ndani ya miezi 12. Ombi lako linapaswa kuashiria muundo wa orodha (kwa mfano, kwenye karatasi au kielektroniki).

**Haki ya Kuomba Vizuizi:** Unaweza kutuomba tusitumie au kufumbua taarifa fulani za kiafya kwa ajili ya matibabu, malipo au shughuli zetu. Ukilipia mwenyewe huduma au bidhaa ya afya kikamilifu, unaweza kutuomba tusishiriki maelezo hayo na mpango wako wa bima ya afya. Tutasema "ndiyo" isipokuwa tuhitajike kisheria kushiriki taarifa hizo, iwapo zitaathiri huduma yako, au iwapo hatuwezi kutii ombi lako.

**Haki ya Kuomba Mawasiliano ya Siri:** Unaweza kuomba tuzungumze nawe kuhusu masuala ya huduma ya afya kwa njia fulani au katika eneo fulani. Kwa mfano, unaweza kuomba tuwasiliane nawe tu kazini au kupitia barua. Tutakubali maombi yote yanayofaa. Unaweza kuomba wakati wa usajili, kwa mwakilishi wa mgonjwa wako, au kwenye Ofisi ya Faragha. Tunaweza kukuomba uandike ombi lako.

**Haki ya Kuomba Nakala ya Karatasi ya Ilani Hii:** Unaweza kuomba nakala ya ilani hii wakati wowote. Hata kama ulikubali kupokea ilani hii kwa njia ya kielektroniki, bado una haki ya kupata nakala ya karatasi. Unaweza kupata nakala ya ilani hii kwenye tovuti yetu, **corewellhealth.org/policies**, au katika kituo chochote cha Corewell Health.

## Mabadiliko kwenye Ilani Hii

Tuna haki ya kubadilisha ilani hii. Pia, tuna haki ya kuanza kutumia ilani iliyorekebishwa kwenye taarifa za kiafya ambazo tayari tunazo na taarifa zozote tutakazopokea baadaye. Tutachapisha nakala ya ilani ya sasa katika vituo, ofisi, na maeneo yanayoshughulikiwa na ilani hii. Ilani hii itakuwa na tarehe ya kuanza kutumika. Pia, nakala ya ilani mpya zaidi itapatikana kwako kila wakati unapojisajili katika kituo au ofisi, au unapolazwa katika kituo kwa ajili ya matibabu, au huduma za kiafya kama mgonjwa aliyelazwa au wa kutwa.

Iwapo unaamini kuwa haki zako za faragha zimekiukwa, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Corewell Health au kwa katibu wa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu Department of Health and Human Services.
Ili kuwasilisha malalamiko kwa Corewell Health, tuma barua pepe kwa **privacy@corewellhealth.org** au uwasiliane na:
Corewell Health, Chief Privacy Officer MC168,
100 Michigan Street NE, Grand Rapids, MI 49503.

Lazima malalamiko yote yawasilishwe katika maandishi.
Hutaadhibiwa kwa kuwasilisha malalamiko.

## Matumizi Mengine ya Taarifa Zako za kiafya

Matumizi na ufumbuzi mwingine wa taarifa za kiafya ambayo hayajashughulikiwa na ilani hii au sheria zinazotumika kwa Corewell Health yatatekelezwa tu ukitupa ruhusa yako katika maandishi. Ukitupa ruhusa ya kutumia au kufumbua taarifa zako za matibabu, unaweza kuondoa ruhusa hiyo kwa kutuandikia wakati wowote. Ukiondoa ruhusa yako, hatutatumia au kufumbua taarifa zako za kiafya kwa sababu ulizobainisha katika ruhusa uliyoandika. Hatuwezi kubatilisha ufumbuzi wowote ambao tayari tumefanya tukiwa na ruhusa yako, na tunatakiwa kuhifadhi rekodi zetu za huduma tuliyokupa.

**corewellhealth.org/policies**